

**KWENDA: MWENYEKITI, KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**KUTOKA: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

TAREHE: 7 MEI, 2022

**YAH: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA
MWEZI APRILI, 2022.**

A: MAPATO:

**I. VYANZO VYA MAPATO YA NDANI VYA HALMASHAURI (OWN
SOURCES)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilijiwekea lengo la kukusanya mapato ya **Tzs 9,106,108,000**. Kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2022 zimekusanywa **Tzs 635,835,990.68** sawa na asilimia **6.99** ya Lengo kwa Mwaka. Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022 imeweza kukusanya Jumla ya **Tzs 7,705,008,824.00** sawa na asilimia **84.61** ya lengo la mwaka.

Taarifa mlingano ya mwezi Aprili, 2022

Lengo la Halmashauri kwa mwezi Aprili, 2022 ni kukusanya kiasi cha **Tzs 758,842,333.31** ambapo zimekusanywa **Tzs 635,835,990,68** sawa na asilimia **83.79** ya lengo la mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatao ni mchanganuo wa mlingano wa

Mapato halisi kwa mwezi Aprili, 2022 kama yalivyokusanywa.

Jedwali la Mlingano: Machi 2022- Aprili 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pun gufu,	(%)
1	Machi	758,842,333.51	1,078,309,403.67	319,467,070.16	142.10
2	Aprili	758,842,333.51	635,835,990,68	(123,006,342.83)	83.79

Upungufu wa mapato dhidi ya makisio ya mwezi yametokana na ukweli kuwa mwezi huu sio wa makusanyo ya juu kwa chanzo cha ushuru wa huduma (Lower season)

II RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikisia kupokea Ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya Tzs 32,818,771,000.00 .Kwa mwezi Aprili, 2022 fedha zilizopokelewa ni Tzs 3,082,154,766.60 sawa na asilimia 9.40 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha Halmashauri ilitarajia kupokea jumla ya Tzs 2,734,897,583.33 kwa mwezi, ambapo kiasi kilichopokelewa ni Tzs 3,082,154,766.60 sawa na asilimia 112.70 ya makisio ya mwezi; Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili, 2022 imeweza kupokea Ruzuku toka Serikali Kuu Jumla ya Tzs 24,301,942,371.94 sawa na asilimia 74.05 ya lengo la mwaka.

Ruzuku iliypokelewa kwa mwezi Aprili, 2022 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

JUMLA YA MAPATO YA RUZUKU: Machi 2022-Aprili 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pungufu,	(%)
1	Machi	2,734,897,583.33	2,244,773,002.43	(490,124,580.90)	82.08
2	Aprili	2,734,897,583.33	3,082,154,766.60	347,257,183.27	112.70

Fedha za ruzuku zilizopokelewa ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida , elimu bila malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari, MDH. TB, na Mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Kibada.

B: MATUMIZI:

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni 2022 Halmashauri imekisia kutumia Tzs. 41,924,878,999.76 kati ya fedha hizo Tzs 32,818,771,000.00 ni kwenye maeneo ya Ruzuku; na Tzs. 9,106,108,000.00 ni katika maeneo yasiyo ya Ruzuku.

Matumizi halisi kwa mwezi Aprili 2022, ni Tzs 2,984,660,357.92 sawa na asilimia 7.12 ya bajeti yote ya matumizi ya mwaka .Aidha matumizi ya ruzuku kwa Mwezi Aprili, 2022 ni Tzs 2,296,773,638.77 sawa na asilimia 7.00 ya bajeti ya mwaka.

Matumizi ya vyanzo vya ndani kwa mwezi Aprili, 2022 ni Tzs 687,886,719.15 sawa na asilimia 7.56 ya bajeti ya mwaka.

Aidha Halmashauri kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili, 2022 imeweza kutumia jumla ya Tzs 28,068,945,589.71 sawa na asilimia 66.95 ya lengo la mwaka.

Mchanganuo wa matumizi ya Fedha Mwezi Aprili, 2022 ni kama ifuatavyo:

▪ Matumizi maeneo yasiyo ya ruzuku	Tzs	687,886,719.15
▪ Matumizi maeneo ya Ruzuku	Tzs	2,296,773,638.77
Jumla	Tzs	2,984,660,357.92

Matumizi yaliyofanyika ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa elimu msingi na sekondari, MDH, na matumizi ya vyanzo vya mapato ya ndani. Jedwali "A", "B" "C" na "D" ikionyesha muhtasari Mapato, Matumizi, mchanganuo wa taarifa mlingano wa mapato ya ndani wa mwezi Aprili, 2022 na mchanganuo wa matumizi (itemized),
Nawasilisha,

Jenoviva Meshi
**K.N.Y: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**